# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA THELATHINI NA TATU

**27 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA THELATHINI NA TATU - TAREHE 27 MEI, 2025

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**417 MHESHIMIWA SALIM MUSSA OMAR (GANDO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali haioni haja ya kutengeneza Kanuni zitakazoweka kima cha chini cha mishahara ya Wafanyakazi wa Majumbani.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**418 MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ukarabati wa Vituo vya Afya Mkalama na Kinyangiri ambavyo ni chakavu.

**419 MHESHIMIWA DKT. MEDARD MATOGOLO KALEMANI (CHATO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya Kata za Nyamilembe, Kasenga na Ilyamachele vilivyoanza kujengwa kwa nguvu za Wananchi.

**420 MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Vituo vya Afya Kitaya na Majengo - Nanyamba vitapatiwa Magari ya kubeba Wagonjwa.

**421 MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Vijiji vyenye maeneo ya Mnada havipati mgao wa asilimia 20 ya mapato ya Mnada.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**422 MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY MAGANGA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ajira kwa Wahitimu wa Vyuo nchini.

**423 MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na upungufu wa Watumishi hususan Walimu na Watoa Huduma za Afya - Newala Vijijini.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**424 MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX (BUHIGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya Mkoa wa Kigoma kuwa lango la biashara.

**425 MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali imefanya tathmini gani ya Vinywaji ilivyoruhusu kama Pombe kuona kama havina athari kwa Wananchi hasa Vijana.

**WIZARA YA UJENZI:**

**426 MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Daraja la Mtomoni.

**WIZARA YA KILIMO:**

**427 MHESHIMIWA AYSHAROSE NDOGHOLI MATTEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Zao la Kitunguu linawanufaisha Wananchi wa Mkoa wa Singida.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**428 MHESHIMIWA DKT. PAULINA DANIEL NAHATO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma ya TEHAMA maeneo wanayotumia Wanafunzi kujisomea katika Vyuo Vikuu vya Umma.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**429 MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali imefikia wapi katika utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu Ushirikiano kati ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Manispaa – Moshi Mjini.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**430 MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA (CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa Wananchi hususan Wafugaji wanaolisha Mifugo maeneo ya Hifadhi ya Reli.

**431 MHESHIMIWA JANETH ELIAS MAHAWANGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, mafunzo gani yanatolewa na Serikali kwa Wanawake Wajasiriamali kuhusu usimamizi wa biashara za uchukuzi na mbinu bora za usafirishaji.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **27 MEI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |